**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule: 0753640908**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0757304209**
**Matron: 0752343174**

**Shule ya Sekondari Jenista Mhagama**
**S.L.P 70**
**Peramiho-Songea**
**Tareha ...........................**

**Kumb: Na. JMS/UT/01/03**
**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………...**
**……………………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JENISTA MHAGAMA HALMASHAURI YA SONGEA MKOA RUVUMA MWAKA .............................**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ....................... na atasoma tahasusi ya ……………...

Shule ya Sekondari **Jenista Mhagama** ipo umbali wa Kilometa 37 Magharibi mwa Mji wa Songea. Usafiri wa basi kutoka mjini Songea unapatikana katika kituo cha mabasi cha Songea. Nauli ni Shilingi 1,500/= hadi Peramiho Hospitali na kutoka hapo kuna umbali wa km.7 Kaskazini hadi shuleni kwa pikipiki ni Shilingi 4,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ....../....../........, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ...../...../.......... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……/……/.......

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**1.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni kijani kibichi (dark green) namba 1 na mwanafunzi anatakiwa awe na sketi mbili zenye mshono wa rinda box mbele na nyuma, iwe na utepe mweupe wenye upana wa sentimeta 3 upande wa chini na iew ndefu mpaka kwenye ugoko wa kisigino. Utepe uwekwe baada ya sentimita 10 kutoka chini.

ii. Mashati meupe mawili mikono mifupi yenye kola ya kijani kibichi, yenye utepe wa kijani kibichi, pia iwe na utepe wa kijani kibichi kwenye mdomo wa mfuko wa shati. Rejea picha iliyoambatanishwa.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ifanane na rangi ya shati la shule ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. (Kwa wanaovaa hijabu na isiwe na urembo au mapambo).
iv. Sare ya Michezo ni Track suit 2 rangi ya kijani kibichi, T-shirt na bukta vyote rangi ya kijani kibichi na raba nyeupe jozi mbili.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi.
vii. Sweta rangi ya kijani kibichi (dark green) yenye shingo ya ”V”.
viii. Nguo za kushindia ni Gauni rangi ya dark bluu mshono wa solo ndefu mpaka kwenye ugoko wa kisigino cha mguu.
ix. Tisheti (T-shirt) rangi ya njano iwe na kola.
x. Shuka mbili za rangi ya pinki.
xi. Blanket moja.

NB: T-shirt,Track suit na sweta zenye nembo ya shule zinapatikana kwenye maduka yaliyopo karibu na shule kwa wale watakaohitaji kununua shuleni.

(a) T-shirt-Tsh. 15,000/=
(b) Truck suit-Tsh. 27,000/=
(c) Sweta- 15,000/=

**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari makubwa 10(kaunta books quire 4.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi (**aina ya double A**) bunda Mbili (2) kwa muhula.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa Tahasusi ya PCB na CBG.
v. Scientific Calculator kwa Tahasusi ya PCB, CBG, HGK na HGL.
vi. Godoro futi $2^1/_2$.
vii. Chandarua 1 rangi ya blue.
viii. Nguo za ndani za kutosha.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Jembe moja lenye mpini.
xii. Fyekeo au reki moja.
xiii. Fagio 1 la uwanjani.
xiv. Brash 1 ya kudekia (hard broom) na mopa 1 (wanafunzi wa PCB, HKL na HGL)

xv. Sofy broom 1 na mopa 1( wanafunzi wa CBG na HGK).
xvi. Begi la kubebea daftari (school bag).
xvii. Dumu la kuhifadhia maji ya kunywa la lita tano rangi nyeupe.
xviii. Solata moja kwa tahadhari **UMEME UNAPOKATIKA.**
xix. Nakala ya result slip ya kidato cha nne pamoja na nakala ya cheti cha kuzaliwa.
xx. Saa ya mkononi.
xxi. Fedha za matumizi binafsi.
xxii. Sanduku imara linalofunga vizuri. (tranker).
xxiii. Laboratory coat moja kwaajili ya majaribio wanapokuwa maabara.
xxiv. File moja. (Box file)

NB: Vifaa vya usafi kama vile jembe, mopa, soft broom, fyekeo, brush, fagio vinapatikana karibu na maduka yaliyopo karibu na shule.

**1.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango ilipwe kwenye akaunti namba: 61810059992 BENKI YA NMB**
**Jina la akaunti: Jenista Mhagama Secondary School.**

**2.Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Wanafunzi watakaokuwa wanapata daraja la nne na sifuri kwenye mitihani ya ndani na nje ya shule watabaki shuleni kipindi cha likizo.
xiii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni. Pia wanafunzi hawaruhusiwi kunyoa mtindo.

**MUHIMU:**

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

- ❖ Fedha taslimu sh. 50,400/= kwa ajili ya Bima ya afya kwa kila mwanafunzi na kwa wanafunzi waliofikisha miaka 18 iambatanishwe na namba ya NIDA kama anayo. (Hii itawahusu wanafunzi wasio na BIMA).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
vii. Uvutaji wa sigara.
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.

ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
x. Kusababisha mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**2. Viambatisho na Fomu Muhimu**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana Jenista Mhagama sekondari.



Felister B. Luambano
Mkuu wa Shule




**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumeikuba tabia ya watu kuwapigia simu wazazi kuwajulisha changamoto za watoto wao ambazo sio rasmi. Hivyo ukipigiwa simu tafadhari usifanye chochote kabla ya kuwasiliana na uongozi wa shule kwa namba zifatazo:-**

- **Mkuu wa shule 0753640908**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0757304209**
- **Mwandamizi Taaluma 0625368331**
- **Mwandamizi Malezi 0620546373**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**JENISTA MHAGAMA SECONDARY SCHOOL**

To the Medical Officer
.................................................
.................................................
.................................................

Please examine the above named student to her/his fitness to pursue secondary education course

____________

**FELISTERLUAMB**
**ANO**
**HEADMISTRESS**

1. Eyes ..................................................................................................
2. Ears ..................................................................................................
3. Mouth ...............................................................................................
4. Heart ................................................................................................
5. Abdomen ..........................................................................................
6. Blood ................................................................................................
7. Urine ..................................................................................................
8. Sputum ..............................................................................................
9. Hb .......................................................................................................
10. Leucocytes .......................................................................................
11. E.S.R ................................................................................................
12. Pregnancy ........................................................................................

Date: ........................................... Signature: .....................................

**MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by the Medical Officer)**
I have examined the above named and consider that she/he is mentally and physically fit for studies.

Signature: .............................. Date: .........................
Designation: ........................... Station ........................

**JINA LA MWANAFUNZI ...............................................................................**

**KIDATO CHA ................................... TAHASUSI YA ......................................**

**NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao hii itasaidia kutoa taarifa endapo tatizo litatokea. Hatutaki majina ya Ndugu bandia. Tunaomba mzingatie hilo kwa ajili ya usalama wa mtoto wako

| |
|---|
| *Picha ya mama/* |

1. (a) Jina .............................................................
   (b) Uhusiano .......................................................
   (c) Anuani ..........................................................
   (d) Namba ya simu .............................................

| |
|---|
| *Picha ya Baba/M* |

2. (a) Jina .............................................................
   (b) Uhusiano ......................................................
   (c) Anuani ..........................................................
   (d) Namba ya simu .............................................

| |
|---|
| *Picha ya Ndugu* |

3. (a) Jina .............................................................
   (b) Uhusiano ......................................................
   (c) Anuani ..........................................................
   (d) Namba ya simu .............................................

| |
|---|
| *Picha ya Mzazi/* |

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ..................................................
Tarehe ......................................................................

**AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU**

Mimi ............................................................. nakubali nafasi niliyopata katika shule ya SEKONDARI JENISTA MHAGAMA kuendelea na masomo ninafahamu kuwa wazazi wangu ndio watakaogharimia masomo yangu, nahaidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidii na nitakuwa mwanafunzi mwaminifu katika kutimiza na kufuata sheria za shule na kushirikiana na wenzangu katika shughuli zote za shule.

| |
|---|
| *Picha ya Mwan* |

..............................

**Sahihi ya Mwanafunzi**

Mimi Mzazi/Mlezi wa ..................................................................... nimesoma yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampa mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua zote zinazomhusu mtoto wangu, nitalipa karo ya shule na michango yote inayotakiwa kwa wakati wake.

Barua na ripoti zinazomhusu mtoto wangu zitaletwa kwangu kwa anwani hii S.L.P ...........................................................................

Jina na sahii ya Mzazi/Mlezi ........................................Tarehe………………………..

Namba ya simu...........................................................

**FOMU NA. 3. KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI**

**A. MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (Matatu)............................................................................
2. Shule ya O-level aliyosoma ..................................................................
3. Namba ya mtihani ...........................................................................
4. Tarehe ya kuzaliwa ...........................................................................
5. Nakubali nafasi niliyopewa/sitaki apewe mwingine (Kata lisilohusika)
6. Nakiri naahidi kutomiliki simu shuleni, kutoshiriki katika migomo, fujona makosa ya jinai kama ilivyo ainishwa katika sheria zashule


7. Sahihi.........................................................................................

**B. MZAZI/MLEZI**


- Nakubali mwanafunzi apate Elimu yake hapo Jenista Mhagama Sekondari
- Na kwamba atafuata sheria na maelekezo yote. Vinginevyo aadhibiwe
- Na kwamba mwanafunzi alelewe katika dini ya....................................
- Sitampa simu mimi binafsi na Ndugu wote wala kuafiki yeye kuwa nayo
- Na kwamba pia nitatekeleza masharti/mahitaji yote yaliyoainishwa na kwamba nitalipa michango yote kwa wakati bila usumbufu wowote
- Na kwamba sitomhamisha mwanangu bila sababu ya msingi

Jina la Mzazi/Mlezi .............................. Nambaza simu ......................

Anuani .............................. Kijiji/Mtaa....................................Sahihi ya Mzazi/Mlezi ......................................... tarehe ............................................



**FELISTER LUAMBANO**
**MKUU WA SHULE**



**MWANAFUNZI**

Jina la Mwanafunzi: (Matatu) .......................................................................................
Tarehe ya kuzaliwa .......................................................................................................
Jinsia ..........................................................................................................................
Umri ........................................................................................................................... Nyumba

(Kitongoji) ...................................Wilaya ....................Mkoa ....................

Simu ya Mzazi/Mlezi .......................................................................................
Jina la Baba/Mlezi ................................Uhusiano ...................Yupo hai? .................
Jina la Mama/Mlezi .............................Uhusiano .....................Yupo hai? ................ Anuani

yake.........................................................................................................

Kazi ya Mzazi/Mlezi..........................................................................................
Umechaguliwa kuingia kidato cha tano/mchepuo/Tahasusi ........................................ Shule

uliyotoka ............................ Ipo Wilaya ya .....................Mkoa ......................

Tarehe ya kuripoti shule ya sekondari Jenista Mhagama
.........................................................................
Ndugu yako wa karibu aliopo

1. Songea Mjini ni (Jina) ........................................................................................
   Uhusiano naye .......................................................................................
   Anuani yake .............................................. Simu na ....................................

2. Mbinga Mjini ni (Jina)......................................................................................
   Uhusiano naye .......................................................................................
   Anuani yake ........................................... Simu na. .......................................

3. Mahali pengine ndani ya Mkoa wa Ruvuma
   Jina .................................................. Namba ya simu
   .................................Uhusiano ..............................................

Mimi .......................................................... nakiri kwamba taarifa nilizotoa ni sahihi Sahihi
................................................... tarehe ............................................

**NB: ENDAPO MWANAFUNZI ATATOA TAARIFA ZISIZOSAHIHI ATACHUKULIWA HATUA ZA KINIDHAMU.**

## OROBHA YA VITABU

(Orodha hiyo ya vitabu unatakiwa kuwa navyo).

**A. PHYSICS**

- Physics for Advanced secondary schools. Student's Book Form Five. (TIE).
- Principles of Physics. (S. CHAND-XI)
- Mastering Physics 1&2.

**B. CHEMISTRY**

- General chemistry for Advanced secondary schools. Student's Book Form Five and Six. (TIE).
- General and Inorganic Chemistry for Advanced secondary schools. Student's Book Form Five and Six. (TIE).
- Physical Chemistry for Advanced secondary schools. Student's Book Form Five and Six. (TIE).

**C. BIOLOGY**

- Biology for advanced secondary schools. Student's Book Form Five.

**D. HISTORY**

- History for Advanced secondary schools. Student's Book Form Five. (TIE).

**E. GEOGRAPHY**

- Physical Geography for advanced secondary schools. Student's Book Form Five and Six. (TIE)
- Practical Geography for secondary schools. Student's Book Form Five and Six. (TIE).

**F. ENGLISH LANGUAGE**

- English for Advanced secondary schools. Student's Book. Form Five. (TIE)
- English for Advanced secondary schools. Student's Book. Form Five. (TIE).

**NOVELS**

- Animal Farm- George Orwell.
- Chasing the Leopold Finding the Lion -Julie Wkeman-Linn.
- The Opportunist Elite – Nyambari Nyangwine
- The Horizon Unveiled – Fellowes Mwaisela.

**PLAYS**

- The Government Inspector- Nikolai V. Gogol.
- An Enemy of the People- Henrick Ibsen
- A Test of Heaven- Farouk Topan.

**POETRY**

- Summons: Poems from Tanzania – Richard S. Mabala.
- Poets of Africa: Lament of the Silent & Other Poems – Jared Angira.

**G. KISWAHILI**

- Kswahili shule za sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano. (TIE).

**RIWAYA**

- Dunia Uwanja wa Fujo – Euphrase Kezilahabi.
- Ua la Faraja – W.E. Mkufya.
- Mirathi ya Hatari – C.G. Mng'ong'o.
- Wasifu wa Siti Binti Saad – Shaaban Robert.

**TAMTHILIYA**

- Mukwav awa Uhehe -M.M. Mlokozi.
- Shujaa Mirambo – Emmanuel Mbogo.
- Usaliti Mjini – Francis Imbunga.

**USHAIRI**

- Fumbo Linaloelea- Nyambari Nyangwine.
- Malenga wa Ziwa Kuu – Wallah Bin Wallah
- Andamo, Msafiri Safarini – Mohammed Khelef Ghassani.
- Wosia wa Baba – Ahmed Mohamed Amanzy.

**H. ACADEMIC COMMUNICATION**

- Academic communication for Advanced secondary schools. Student's Book Form Five. (TIE)
- Academic communication for Advanced secondary schools. Student's Book Form Six. (TIE

**I. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI.**

- Historia ya Tanzania na Maadili shule za sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano. (TIE).
- Historia ya Tanzania na Maadili shule za sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Sita. (TIE).

J. BASIC APPLIED MATHEMATICS.


- Basic Applied Mathematics for Advanced secondary Schools. Student's Book Form Five. (TIE).

**NB:** Kwa maelekezo zaidi ya upatikanaji wa vitabu wasiliana na mwalimu wa taaluma **Mr. Henjewele** (0625368331/0764478145).

# KIAMBATANISHO CHA SARE ZA SHULE



SWETA



SHAMBA DRESS



HIJABU



T-SHETI



TRACK , SHATI NA SKETI